TOLEO Na. 03 | Disemba, 2025

# PBPA Bulletin



Mhe. Deogratius Ndejembi
Waziri wa Nishati

## Waziri wa Nishati Atoa Wito wa Kuongeza Akiba ya Mafuta

PbpaTanzania   PbpaTanzania   pbpa_tanzania

# KAMATI YA UHARIRI

1. **Lilian Rwegimbura**
   Mwenyekiti
2. **Sarah Mwakyusa**
   Katibu
3. **Matiko Sanawa**
   Mjumbe
4. **Henry Kilenga**
   Mjumbe
5. **Rehema Mahundi**
   Mjumbe
6. **Nyamhoni Chacha**
   Msanifu

## Wasiliana nasi

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA),
Sanduku la Posta 2634,
Dar es Salaam, Tanzania,
info@pbpa.go.tz.
+255 222 129 009

# YALIYOMO


04. WAZIRI WA NISHATI ATOA WITO WA KUONGEZA AKIBA YA MAFUTA

05. PBPA YABORESHA UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA MAFUTA NCHINI

08. PBPA: TAASISI ZA MAFUTA ZISHIRIKIANE KULINDA USALAMA NA MAZINGIRA

11. PBPA YAFUNDISHWA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA

13. PBPA YAPATIWA MAFUNZO KUHUSU MAGONJWA YA MOYO, VVU/UKIMWI NA HOMA YA INI

15. PBPA YASHIRIKI MAONESHO YA NANENANE

17. PBPA YASHIRIKI MAONESHO YA BIASHARA YA SABASABA

20. PBPA YABORESHA HUDUMA KUPITIA MFUMO MPYA WA KIDIGITALI

# WAZIRI WA NISHATI ATOA WITO WA KUONGEZA AKIBA YA MAFUTA



**Mhe. Deogratius Ndejembi**
Waziri wa Nishati

Waziri wa Nishati, Deogratius Ndejembi, ametoa wito kwa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhakikisha nchini kunakuwepo na akiba ya kutosha ya mafuta ili kuendeleza shughuli za uzalishaji, usafirishaji na huduma muhimu zinazotegemea nishati hiyo.

Akiwa kwenye ziara ya kikazi katika ofisi za PBPA, Waziri Ndejembi amesema hatua hiyo itaimarisha usalama wa nishati na kuiwezesha nchi kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta. Amesisitiza kuwa PBPA inapaswa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) pamoja na wadau wa sekta binafsi ili kuongeza uwekezaji katika ujenzi wa maghala mapya ya kuhifadhia mafuta.

“Akiba ya mafuta kupitia uwekezaji katika vituo vya kuhifadhi inaleta utulivu wa kiuchumi kwa Taifa. Pale kunapokuwepo na uhakika wa upatikanaji wa mafuta, shughuli za uzalishaji, usafirishaji na biashara zinaendelea bila vizuizi. Hili huongeza imani ya wawekezaji, hupunguza gharama za dharura na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi,” amesema Mhe. Ndejembi.

Ameongeza kuwa matarajio yake ni kuona ongezeko la uwekezaji katika miundombinu ya hifadhi ya mafuta ili nchi iweze kuhifadhi kiasi kikubwa na kuendelea kutekeleza majukumu yake bila changamoto za upatikanaji wa bidhaa za mafuta.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa PBPA, Erasto Simon, amemshukuru Waziri kwa ziara hiyo na kuahidi kuwa wakala utaendelea kushirikiana na wizara ili kuboresha utendaji kazi. Amesema PBPA inaendelea kusimamia mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja kwa ufanisi na kuhakikisha taifa linakuwa na mafuta ya kutosha wakati wote.

Ameongeza kuwa, ili kuboresha zaidi utoaji huduma, PBPA imeanza maandalizi ya kuunganisha mifumo itakayowezesha upatikanaji wa bei linganifu katika bandari zote, jambo litakalosaidia kuongeza ufanisi katika usambazaji wa mafuta

# PBPA YABORESHA UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA MAFUTA NCHINI



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) akiongea na Wahariri na Waandishi wa Vyombo vya Habari katika Mkutano uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa JK Nyerere jijini Dae salaam.*

Serikali kupitia **Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)** imefanikiwa kuboresha upatikanaji, usimamizi, na ufanisi wa mnyororo wa uagizaji bidhaa za petroli (dizeli, petroli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege (JET-A1)) nchini hivyo kuendelea kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hizo na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Akizungumza katika mkutano na Wahariri wa Vyombo vya Habari jijini Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu wa PBPA, Bw. Erasto Simon, alisema mafanikio hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mikakati ya Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Bw. Erasto Simon alisema kuwa Serikali imewezesha kuongezeka idadi ya kampuni zinazoshiriki katika mchakato wa uagizaji mafuta kutoka kampuni 81 mwaka 2021 hadi kufikia kampuni 89 mwaka 2025, sawa na ongezeko la asilimia 9.87. Ongezeko hili ni matokeo ya sera na mazingira mazuri yaliyowekwa kwa wafanyabiashara.

“Wakala umesajili jumla ya wazabuni wapya 8

katika Mfumo wa BPS kwa kipindi cha miaka minne, kuanzia 2021 hadi 2025 hivyo kufanya jumla ya wazabuni waliosajiliwa katika kipindi husika kuwa ni 89 Aidha, idadi ya zabuni za uletaji mafuta imeongezeka kutoka wastani wa 109 mwaka 2021 hadi 118 ifikapo Desemba 2025 sawa ongezeko la asilimia 8," alisema Bw. Erasto Simon.

Alifafanua kuwa PBPA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kupanga ratiba za meli za bidhaa za mafuta ili kuongeza ufanisi wa matumizi ya bandari na kupunguza gharama za kusubiri kwa meli (demurrage costs).

Hatua hiyo imewezesha kuokoa zaidi ya Dola za Marekani milioni 11.5, sawa na Shilingi bilioni 29.95 kwa mwaka fedha ambazo hapo awali zilitumika kulipia gharama za ucheleweshaji wa meli. Hatua hiyo imechangia ongezeko la akiba ya fedha za kigeni nchini.

Aidha, PBPA imeboresha usimamizi wa taarifa za mafuta yanayoingia nchini kupitia mfumo wa BPS na yale yaliyo nje ya mfumo. Kuanzia Julai 2024, wakala umeanza kusimamia na kutunza taarifa za mafuta yote yanayoagizwa nje ya mfumo. Hatua hii imeiwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za mafuta yote yanaoingia nchini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Bw. Sabato Kosuri, alisema Ofisi ya Msajili wa Hazina inatambua mchango wa vyombo vya habari katika kuhabarisha umma na itaendelea kushirikiana navyo kwa karibu ili kudumisha uwazi na uzalendo.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Bw. Deogratius Balile, aliipongeza PBPA kwa mafanikio ya Mfumo wa BPS katika kuboresha upatikanaji wa mafuta nchini, huku akisisitiza umuhimu wa kudhibiti ubora wa mafuta yanayoingia sokoni ili kulinda maslahi ya taifa na watumiaji.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina, Bw. Sabato Kosuri akiwakaribisha Wahariri na Waandishi wa Vyombo vya Habari (hawapo pichani) katika Mkutano wa Wahariri na PBPA uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa JK Nyerere jijini Dar salaam.*

*Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Bw. Deogratius Balil akitoa salamu za shukrani kwa Menejimenti ya PBPA na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kufanikisha mkutano wa Wahariri wa Vyombo vya Habari uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa JK Nyerere jijini Dar salaam.*



*Baadhi ya Watumishi wa PBPA wakiwa katika kikao kazi na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).*



# PBPA: TAASISI ZA MAFUTA ZISHIRIKIANE KULINDA USALAMA NA MAZINGIRA



*Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) Kigoma, akitoa taarifa ya utekelezaji wa Kazi za Bandari upande wa Mafuta kwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi PBPA (hawapo pichani).*

Bodi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) imetoa wito kwa taasisi zote zinazohusika na usimamizi wa mafuta nchini kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha taratibu za upakiaji na upakuaji mafuta zinafanyika kwa kuzingatia kanuni za usalama na uhifadhi wa mazingira.

Wajumbe wa Bodi wametoa kauli hiyo wakati wa ziara ya kukagua huduma za shehena za mafuta katika Bandari za Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma. Walisema kuwa upakiaji wa mafuta bila kutumia mifumo rasmi ni hatari, kwa kuwa unaweza kuharibu mazingira na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya PBPA, Dkt. Lutengano Mwakahesya, alisema kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha miundombinu yote ya kusafirisha mafuta imejengwa kwa kuzingatia viwango vya usalama.

"Kushusha mafuta moja kwa moja kutoka kwenye malori hadi melini bila kupitia kwenye maghala ya kuhifadhia mafuta ni hatari. Tunashauri TPA iangalie uwezekano wa kujenga maghala mapya ya

kuhifadhia mafuta au kuboresha yaliyopo kupitia maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Kigoma," alisema.

Aliongeza kuwa ni vyema TPA ikaweka utaratibu wa bei sawa (equal pricing) kwa shughuli zote za kushusha na kusafirisha mafuta kupitia Kigoma ili kurahisisha matumizi ya maghala ya kuhifadhia mafuta, kupunguza gharama kwa wadau na kuongeza usalama wa shughuli hizo.

Awali akiwasilisha taarifa ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) Kigoma, Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Edward Mabula, alisema kwa sasa bandari hiyo inatumia mfumo wa "dipping", huku maandalizi ya kuanza kutumia mita za kupimia kiwango cha mafuta zenye ufanisi zaidi yakiendelea.

Bw. Mabula alisema biashara ya mafuta katika bandari hiyo imekuwa ikikua mwaka hadi mwaka. "Kwa mfano, mafuta yaliyopokelewa yameongezeka kutoka tani 32,826 mwaka 2023 hadi tani 52,367 mwaka 2024. Hii inaonyesha jinsi uhitaji wa huduma unavyoongezeka," alisema.

Alifafanua kuwa mafuta hayo yanapokelewa kupitia maghala ya kuhifadhia mizigo na kusafirishwa kwa meli kwenda nchi jirani za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Aidha,TPA imejipanga kuhakikisha kuwa mafuta yanayopokelewa katika bandari hiyo kwa ajili ya kupelekwa nchi jirani yanasafirishwa kwa wakati.


Kwa upande wake, Meneja Msadizi wa Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bandari za Ziwa Tanganyika, Mohamed Mnonda, alisema taasisi yake kwa kushirikiana na TPA, EWURA na wadau wengine inasimamia kwa karibu mizigo yote inayosafirishwa nje ya nchi kupitia Kigoma.

"TRA inahakikisha mizigo yote inapimwa na kusajiliwa ipasavyo ili kuepusha upotevu wa mapato ya Serikali na kulinda usahihi wa takwimu za biashara," alisema.

Serikali kwa sasa inaendelea na maboresho ya bandari za ziwa Tanganyika, lengo likiwa ni kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena kubwa za mafuta na bidhaa nyingine. Maboresho hayo yanatarajiwa kuongeza ushindani wa bandari za Tanzania katika ukanda wa Maziwa Makuu na kusaidia kukuza biashara na usafirishaji kwenda nchi jirani za Burundi, Congo na Zambia.



*Wajumbe wa Bodi ya Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakikagua eneo la kupakia mafuta Kwenda kwenye Meli katika Bandari ya Kigoma.*




*Meneja Msadizi wa Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bandari za Ziwa Tanganyika, Mohamed Mnonda, akitoa taarifa ya utekelezaji kwa kwa Wajumbe wa Bodi ya PBPA (hawapo pichani)*



*Picha ya Pamoja ya Wajumbe wa Bodi ya PBPA na Watendaji wa TPA Bandari ya Kigoma.*

# PBPA YAFUNDISHWA MKAKATI WA TAIFA DHIDI YA RUSHWA



*Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Wilson Nyamanga, akitoa mafunzo kuhusu Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne (2023–2030) kwa watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).*

Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Utawala kutoka Wizara ya Nishati, Bw. Wilson Nyamanga, ametoa mafunzo kuhusu Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne (2023–2030) kwa watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA.)

Nyamanga alitoa mafunzo hayo jijini Dar es Salaam na kusema kuwa lengo la mkakati huo ni kuwajengea watumishi maadili bora na uelewa wa namna ya kukabiliana na vitendo vya rushwa katika maeneo ya kazi.

Mkakati huo unalenga pia kuwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa, kwa kujenga uwezo na ari kwa wananchi kudai uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma. Vilevile, unaelekeza juhudi katika kuimarisha uwajibikaji na uwazi ndani ya taasisi za Umma na zisizo za kiserikali, sambamba na kuimarisha kazi za Kamati za Uadilifu kama

nyenzo muhimu za kudumisha maadili kazini.

Aidha, Bw. Nyamanga alibainisha kuwa Taasisi za Utawala Bora kama Ofisi ya Rais-Ikulu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, TAKUKURU, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, zina jukumu muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wa Mkakati huo unafanyika kwa ufanisi.

Miongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mkakati wa Awamu ya Nne ni kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa umma ili kupunguza mianya ya rushwa. Matumizi ya mifumo ya kidigitali yanatajwa kusaidia kuondoa mahusiano ya ana kwa ana kati ya mtoa na mpokea huduma, hatua inayochangia kuongeza uwazi na ufanisi.

Mkakati huo pia unasisitiza ushirikiano wa wadau mbalimbali, zikiwemo asasi za kiraia, sekta binafsi, taasisi za dini, tasnia ya habari, na washirika wa maendeleo, katika juhudi za kukuza uadilifu na kupambana na rushwa.

Mafunzo hayo yamepokelewa kwa hamasa kubwa na watumishi wa PBPA, wakiahidi kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na uwazi, sambamba na kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa.





*Baadhi ya Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mfuta kwa Pamoja katika mafunzo kuhusu Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne (2023–2030) yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano Ofisi ya Wakala jijini Dar es Salaam.*




*Dkt. Hafidh Ameir kutoka Mamlaka ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), leo ametoa mafunzo ya VVU/UKIMWI na Homa ya Ini kwa watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA). Mafunzo hayo yamefanyika jijini Dar es Salaam kwenye ofisi za Wakala.*

# PBPA YAPATIWA MAFUNZO KUHUSU MAGONJWA YA MOYO, VVU/ UKIMWI NA HOMA YA INI

Watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wamepatiwa mafunzo kuhusu magonjwa ya moyo, VVU/UKIMWI na Homa ya Ini. Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa ofisi za wakala jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuboresha afya na ustawi wa watumishi.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Dkt. Janeth Mmari kutoka Taasisi ya Moyo ya



*Baadhi ya Watumishi wa PBPA walioshiriki mafunzo ya VVU/UKIMWI na Magonjwa ya Moyo yalifanyika jijini Dar es Salaam kwenye ofisi za Wakala.*

Jakaya Kikwete (JKCI) alieleza kuhusu kinga na udhibiti wa magonjwa ya moyo. Aidha alibainisha kuwa magonjwa hayo yamekuwa yakiongezeka kutokana na mabadiliko ya mtindo wa maisha.

Dkt. Mmari aliwahimiza watumishi kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara, kuepuka vyakula vyenye mafuta mengi na chumvi kupita kiasi, pamoja na kufanya mazoezi angalau mara tatu kwa wiki. Alisisitiza pia umuhimu wa kupunguza msongo wa mawazo, kutumia muda wa mapumziko ipasavyo, na kuzingatia lishe bora kama njia ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.



*Baadhi ya Watumishi wa PBPA walioshiriki mafunzo ya VVU/UKIMWI na Magonjwa ya Moyo yalifanyika jijini Dar es Salaam kwenye ofisi za Wakala.*



*Dkt. Janeth Mmari kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) akitoa mafunzo kuhusu Magonjwa ya Moyo kwa watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA). Mafunzo hayo yamefanyika katika ukumbi wa mikutano ofisi za Wakala.*

Kwa upande mwingine, Dkt. Hafidh Ameir kutoka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) alitoa mafunzo kuhusu VVU/UKIMWI na Homa ya Ini, akisisitiza umuhimu wa watumishi kuongeza uelewa kuhusu kinga, matibabu, na namna ya kuishi salama kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU.

Alieleza kuwa Homa ya Ini ni miongoni mwa magonjwa hatari yanayoweza kuathiri ini kwa muda mrefu bila dalili za Awali kuonekana, hivyo ni muhimu kuchukua tahadhari mapema. Dkt. Ameir aliwahimiza watumishi kupima afya zao mara kwa mara, kuepuka tabia hatarishi, na kuelimishana kuhusu athari za unyanyapaa kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU.

Watumishi wa PBPA walishukuru kwa mafunzo hayo wakisema yamewapatia maarifa muhimu ya kuboresha afya zao, kuongeza ufanisi kazini, na kuwasaidia kutoa elimu sahihi kwa jamii kuhusu kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na yale yanayoambukiza.



*Mhandisi, Hassan Saidy, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), akiwa katika banda la Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), kwenye maonesho ya Nanenane yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.*

# PBPA YASHIRIKI MAONESHO YA NANENANE

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umeshiriki katika Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma.

Ushiriki wa PBPA katika maonesho hayo unalenga kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake ya msingi, ambayo ni pamoja na uagizaji mafuta, usajili wa wazabuni na OMCs, usimamizi wa mikataba ya uagizaji mafuta, usimamizi wa huduma za upakuaji mafuta, pamoja na uratibu wa mahitaji ya bidhaa za mafuta nchini pamoja na kusimamia bidhaa za mafuta zinazoenda nchi jirani.

Akizungumza katika banda la PBPA, Mhandisi Prudence Laurian alisema kuwa ushiriki wa wakala unatoa fursa kwa wananchi kuelewa kwa undani kuhusu mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System), manufaa yake kwa taifa, na mchango wa PBPA katika kulinda usalama wa nishati ya mafuta nchini.

“Tunatumia jukwaa hili kueleza wadau umuhimu wa bidhaa za petroli katika kuchochea ukuaji wa uchumi kwani husaidia katika kupunguza gharama, kuimarisha upatikanaji wa mafuta, na kuhakikisha sekta za usafirishaji, kilimo, viwanda na huduma nyingine zinapata mafuta kwa wakati,” alisema Mhandisi Prudence.

Aidha, PBPA imeendelea kuweka msisitizo katika kuelimisha wananchi kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa kuhakikisha usalama wa mafuta nchini, ikiwa ni pamoja na kudhibiti upotevu, na kupambana na

uchepushaji wa bidhaa hizo muhimu.

Maonesho ya Nanenane ni jukwaa muhimu la kuonesha mafanikio ya Sekta ya Kilimo na wadau wake, huku yakitoa fursa kwa taasisi mbalimbali za Serikali, Sekta Binafsi, na wananchi kushirikiana katika kuendeleza kilimo na uzalishaji nchini. Kwa PBPA, maonesho haya ni njia mojawapo ya kuonesha namna nishati ya mafuta inavyokuwa sehemu ya mnyororo wa maendeleo ya kilimo.

Maonesho ya 32 ya Nanenane, yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa, yana lengo la kukuza uchumi, kuongeza matumizi ya teknolojia bora na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa. Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo yanahusisha washiriki zaidi ya 1,000 kutoka ndani na nje ya nchi.




*Wataalamu kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakitoa elimu kwa umma kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala katika ya Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.*

# PBPA YASHIRIKI MAONESHO YA BIASHARA YA SABASABA

*Mkurugenzi wa Uendeshaji kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) Mhandisi Bruno Tarimo katika picha ya Pamoja na Wadau wa Mafuta katika Maonesho ya Kibiashara ya Sabasaba yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Jijini Dar es Salaam*




Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umeungana na taasisi nyingine za Serikali na sekta binafsi kushiriki katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu kama Sabasaba, yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Barabara ya Kilwa.

Ushiriki wa PBPA katika maonesho hayo ulilenga kuelimisha umma kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na wakala, pamoja na kuongeza uelewa kuhusu mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS) unatumika kuratibu uagizaji mafuta kwa pamoja nchini.

PBPA ilitoa elimu kuhusu majukumu yake ya msingi katika usimamizi wa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja. Wananchi walipata maelezo kuhusu mchakato wa uagizaji wa mafuta, taratibu za usajili wa kampuni zinazoshiriki kwenye mfumo, usimamizi wa upakuaji wa mafuta kutoka melini na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kuboresha biashara ya mafuta nchini.



*Wataalamu kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakiendelea kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala katika Maonesho ya SabaSaba yanayoendelea jijini Dar es Salaam.*

Aidha, wananchi waliotembelea banda la PBPA walipata nafasi ya kuuliza maswali na kupata majibu kuhusu changamoto mbalimbali zinazohusiana na upatikanaji wa mafuta nchini, pamoja na kujionea machapisho mbalimbali kuhusu shughuli za wakala.

Maonesho ya Sabasaba yamekuwa jukwaa muhimu kwa Wakala kuonesha mafanikio ya Serikali katika Sekta ya Mafuta, sambamba na kuimarisha mahusiano kati ya Wakala na wananchi. Pia maonesho hayo yanatoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kukutana, kubadilishana uzoefu, kutafuta masoko na kujifunza teknolojia mpya.



*Wataalamu kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakiendelea kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala katika Maonesho ya Kibiashara ya Sabasaba yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Jijini Dar es Salaam.*




*Wananchi wakiwa katika banda la Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kupata elimu kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala.*



# PBPA YABORESHA HUDUMA KUPITIA MFUMO MPYA WA KIDIGITALI

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umefanya kikao cha ushirikishwaji wa wadau wa ndani kwa lengo la kukusanya maoni kuhusu mfumo mpya wa kidijitali utakaotumika kusimamia shughuli zake.


Mfumo huo unajulikana kama Bulk Procurement Management Information System (BPS-MIS) unatarajiwa kuboresha kwa kiwango kikubwa utendaji wa PBPA kwa kuongeza uwazi, ufanisi, na uwajibikaji katika mchakato mzima wa uagizaji wa bidhaa za mafuta kwa pamoja nchini.

Akizungumza katika kikao hicho, Afisa TEHAMA wa PBPA, Bw. Moses Mgonja, alieleza kuwa mfumo huo unatarajiwa kuongeza ufanisi kwa kurahisisha michakato yote ya uagizaji kuanzia zabuni, usajili wa kampuni za mafuta (OMCs), uchambuzi wa mahitaji, utoaji wa zabuni, usafirishaji na upokeaji wa mafuta na kufanya maamuzi kwa wakati. Mfumo huu utapunguza makosa ya kibinadamu kupitia teknolojia ya kisasa.

Aidha, mfumo huo utarahisisha ufuatiliaji wa kumbukumbu za zabuni, mikataba, na mawasiliano kwa njia ya kidigitali, jambo litakaloongeza uwazi na kuwasaidia wadau kama EWURA, TRA, TBS, na TASAC kupata taarifa kwa wakati.

Bw. Mgonja aliongeza kuwa kuanzishwa kwa mfumo huo wa TEHAMA ni utekelezaji wa matakwa ya Kifungu cha 18(4) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, inayotaka taasisi zote za umma kutumia mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma na kutekeleza majukumu yake ya kisheria.

“BPS-MIS ni hatua muhimu katika mageuzi ya kidigitali ya PBPA na unatoa mfano mzuri wa matumizi ya teknolojia katika Sekta ya Nishati na biashara ya mafuta nchini. Kupitia mfumo huu, Wakala unaimarisha jitihada za Serikali katika mabadiliko ya kidigitali, ikibadilisha michakato yake kwenda mfumo wa kisasa wa kielektroniki.” Alisema



*Baadhi ya watumishi walioshiriki kikao cha ushirikishwaji wa wadau wa ndani (stakeholder engagement) kwa lengo la kukusanya maoni na mapendekezo kuhusu mfumo wa kidijitali utakaoendesha shughuli za Mamlaka ya Huduma ya Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).*





Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa
Pamoja (PBPA),
Sanduku la Posta 2634,
Dar es Salaam, Tanzania,
info@pbpa.go.tz.
+255 222 129 009

PbpaTanzania PbpaTanzania pbpa_tanzania